SPW IS NOW
RESTLESS DEVELOPMENT
THE YOUTH-LED DEVELOPMENT AGENCY

THIS ISSUE

1 Uongozi wa Wanawake
2 Safari ya Izzy
3 Ofisi mpya Dar
4 Mtukutu mpaka mfano wa kuigwa

KUTOONEKANA NCHINI TANZANIA

UONGOZI WA WANAWAKE

Mwezi March 2012 shirika la Restless Development liliandaa kwa mafanikio mashauriano kwa ajili ya kusaidia uandazi wa mradi wa majaribio unaongazia uongozi wa wanawake (Young Women Leadership Programme)

Kongamano hili liliwakutanisha wanawake wenye usuli tofauti ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa vyuo, wajasiriamali, walio na wasio na ajira

Kongamano lilianza kwa hotuba toka kwa wanawake wenye mafanikio ambao pia ni mfano wa kuigwa kwa washiriki vijana. Uwasilishaji ulihusisha hotuba toka Mheshimiwa Pindi Chana (Mbunge) na mtangazaji maarufu wa kipindi cha “Wanawake Live” Joyce Kiria ambao wote kwa pamoja walitoa hotuba zilizotoa changamoto na kuhamasisha vijana wa kike kuchukua hatua madhubuti kwa maisha yao

Kongamano liliwagawa washiriki katika makundi ili kujadili masuala muhimu yanayowaathiri wanawake na wasichana.

Washiriki walibainisha yafuatayo kama vikwazo vinawakabili wanawake na wasichana

- Kiwango kidogo cha elimu miongoni mwa wanawake
- Kukosena kwa fursa za majikwimu na ajira
- Sheria zenye ubaguzi– wanawake hawamiliki ardhi na rasilimali zingine.
- Mila na utamaduni/dhana potofu
- Kutojitambua miongoni wa wanawake wengi

Ili mradi huu ufanye kazi kifuanisi, washiriki walipendekeza yafuatayo

- Usawa imara wa kijinsia
- Utekelezaji wa sera zinazogusa masual ya wanawake
- Uanzishwaji wa jukwaa la wanawake nchi nzima

SAFARI YA IZZY

Izzy Fairbairn ni mshindi wa tuzo ya Mzalishaji bora wa Vipindi vya Radio inayotolewa na Sony. Ana uzoefu wa juu katika miradi na ujuzi wa kusimamia ushirikiano ndani na nje ya BBC.

Alitembelea Restless Development Tanzania kwa sababu zifuatazo:

- Kuongoza zoezi la upangaji akiwa na wafanyakazi watakaochaguliwa na shirika pamoja na alumnai wetu ili kutambua fursa na uwezo wa kutumia midia jamii kama sehemu ya Mkakati wetu wa Kitaifa
- Kusaidia wafanyakazi kutambua na kuandaa mradi wa majaribio kwa mwaka 2011/2012 ili kusaidia eneo hili la kazi
- Kukutana na wanahabari ili kutathmini fursa na uhai wa mipango yetu.

Akiwa Tanzania, Izzy aliendesha mafunzo ya midia katika uhifadhi na uhariri wa habari sauti. Aliwafunza alumnai wetu wa UDOM jinsi ya kuandaa vipindi vya redio, jinsi ya kurekodi na kuhariri vipindi na jinsi ya kutengeneza matangazo mafupi.

Izzy pia alipata nafasi ya kutembelea kempu yetu ya vijana ya Umoja Dadas. Safari ya Izzy imefanikiwa sana na sisi kama shirika tunajipanga kugawana matunda ya ujio wake na washirika wetu, wafadhili na wahisani pamoja na washikadau wengine

OFISI MPYA DAR

Tumehamia jengo jipya lililo nyuma ya Shoppers Plaza Mikocheni. Mwanzoni tulikuwa Mikocheni karibu na Kairuki Hospital

Tupo ghorofa ya 3, Mtaa wa Chuwaku Kitalu No. 172. Wote mnakaribishwa

FIND OUT MORE

liz@restlessdevelopment.org
Find Restless Development on Facebook
Follow @RestlessDev on Twitter

Restless Development inawaweka vijana katika mstari wa mbele wa mabadiliko na maendeleo nchini Tanzania

TOKA UTUKUTU MPAKA MFANO WA KUIGWA

Daniel*, ambaye aliwahi kuwa kijana mtukutu na mwenye kuogofya, anaishi kata ya Mkumbi mkoani Ruvuma. Alikuwa maarufu kwa tabia zake mbaya na mara nyingi alihusika kufanya vurugu zilizopelekea kupelekwa polisi. Kwa vijana wengi kijijini kwao, Daniel alikuwa shujaa na kiongozi wao. Daniel, ambaye aliwahi kudiriki kuwafukuza na panga viongozi wake wa kijiji eti kwasababu walimtaka abadili tabia, aliwahi kushiriki katika uchaguzi. Hata hivyo, kundi kubwa la jumuiya yake halikumpigia kura

Daniel* alikuwa kikwazo cha uanzishaji Kikundi Kazi cha Jumuiya ambacho vijana wa wanaojitolea toka shirika la Restless Development walikuwa wakijaribu kukianzisha ili kusaidia maendeleo ya vijana katika jumuiya. Alikuwa akiwahamasisha vijana kutokukubali kujiunga na kikundi hicho. Baada ya kukumbana na ugumu katika utekelezaji wa shughuli zao, na baada ya kutambua ushawishi alionao Daniel kwa vijana wa kata ya Mkumbi, vijana wetu wanaojitolea waliamua kutengeneza urafiki na Daniel. Wakaanza kumuhusisha katika shuguli zao za kimaendeleo na moja kwa moja vijana wengine wakaanza kuvutika na kushiriki.

DANIEL MPYA

Daniel* kwa sasa mjumbe wa kamati ya wilaya inayoundwa na vijana watano. Kazi yao ni kuanzisha na kusimamia baraza la vijana ambalo halikuwepo hapo kabla

Akiwa kama mjumbe, Daniel na wenzake wamefanikiwa kuvisadia Vikundi Kazi vya Jumuiya kupata usajili wa kamili wa CBO

Maendeleo haya yameifanya jumuiya yake kukuamini. Na hata pindi mmoja wa vijana wanaojitolea alipoondoka, aliteuliwa yeye kuziba nafasi hiyo. Februari 2012, akiwa kama kiongozi wa vijana wanaojitolewa wa jumuiya alishiriki katika mafunzo yaliyofanyika Songea. Alijifunza mambo mengi sana ambayo sasa anawafundisha vijana wenzake pia.

Daniel* ameamua kuhamasisha vijana wenye tabia alizokuwa nazo yeye kubadilika. Viongozi wa jumuiya ambao walikumbana adha za vurugu za Daniel hapo kabla, wameahidi kumpa ushirikiano katika shughuli zote anazopanga kufanya akiwa kama kijana anayejitolea.

DANIEL MFANO WA KUIGWA

Asha* ni miongoni wa vijana waliohamishwa na Daniel. Anatoka kwenye familia masikini sana, na alikuwa akijihusisha na mahusiano na wanaume wengi ikiwa kama njia ya kujipatia kipato. Asha alipata mimba ambayo hakujua baba ni nani. Kuona hivyo, akaamua kuitoa kwa njia za kienyeji na almanusra apoteze maisha yake.
Baada ya Daniel* kusikia matatizo yanayomkabili Asha, alioomba kuongea naye. Mazungumzo hayo ndio hasa yaliyobadili maisha ya Asha. Kupitia Daniel, Asha amejifunza kuhusu VVU/UKIMWI, uzazi wa mpango na majikwimu. Daniel* pia alimshauri kupima VVU kitu ambacho Asha alikubalina nacho.

Asha* kwa sasa anaishi na mtu anayempenda kwa dhati na wamefanikiwa kupata mtoto wa kikes. Wapenzi hawa wamenunua shamba ambalo wamepanga kulifanyia mradi wa kujiongezea kipato. Daniel* ndiye muhamasishaji mkuu wa mipango anayofikia Asha na pia Daniel anaendelea kutoa elimurika kwa Asha.

Majina yamebadilishwa kulinda utambulisho

FIND OUT MORE

liz@restlessdevelopment.org
Find Restless Development on Facebook
Follow @RestlessDev on Twitter